



WALIMU WAKUU WAPATIWA MAFUNZO MAALUM YA MFUMO WA KURATIBU TAARIFA ZA WANAFUNZI (SIS) KWA KUTUMIA TABLETS

Akizindua Mafunzo hayo yaliyo ratitbiwa na OR Tamisemi kwa kushirikiana na Equip Tanzania Kaimu Mkurugezi wa Halmashauri ya Itilima Bi. Pendo Haule aliwataka Walimu hao kufuatilia mafunzo hayo kwa makini ili waveze kuten-geneza na kutuma taarifa zilizo sahihi.

Aidha Bi. Upendo alisema "Dunia inabadili-ka kwa kasi sana na Tan-zania ya leo ni tofauti na ile ya zamani tunaelekea katika (e Government)

matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika kutoa huduma mbalimbali za serikali , sasa basi ni Matarajio



Kutokea kulia Kaimu Mkurugenzi Itili-ma Bi upendo Haule , wa kwanza kulia afisa Elimu (w) Itilima Ndg Christophe Hirali , kutokea Kushoto Ni Wakufunzi kutoka Tamisemi Deogratias Kashindye, Hemed Mkupa na Amina Kulwa

yangu mtafuatilia mafunzo haya kwa umakini".

Mmjoa wa wawezeshaji Kutoka Tamisemi Ndg. Hemed Mkupa aliwataka walimu waachane na kuten-geneza taarifa ambazo si sahihi

"taarifa ambazo mnataki-wa kuzituma ni Muhimu sana kwa ustawi wa Elimu nchini na ni lazima mfa-hamu umuhimu wa kupata mafunzo haya, kwani taarifa ambazo tamisemi hawana, afisaelimu mkoa na wilaya hawana, ila wewe Mkuu wa shule unazo, unalazimika kufuatilia mafunzo kwa umakini ili taarifa za kuusu shule na Wanafunzi zitumwe kwausahihi" alisema Mkufunzi huyo.



Kushoto Wakuu wa shule za Msingi Wilayani Itilima Wakimsikiliza Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Itilima Bi Upendo Haule Hayup katika Pichani



Wakuu wa Shule za Msingi Wilayani Itilima wakiwa katika vipondi vya Darasani wakielekezwa jinsi ya ku-tumia Mfumo wa SIS kwa kutumia Vishikwambi (tablets)